

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

Mkoa wa Dodoma
Anwani ya Simu REGCOM
Simu Nambari:
2324343/2324384
E-Mail No. ras@dodoma.go.tz
Fax No. 255 026 2320046



Ofisi ya Mkuu wa Mkoa
S.L.P. 914
DODOMA

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI


Aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Ndg. Jordan Rugimbana, Leo Oktoba 30, 2017 amemkabidhi rasmi ofisi Mkuu mpya wa Mkoa wa Dodoma Mhe. Dkt. Bilinith Mahenge mbele ya Wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Dodoma, Wakuu wa Wilaya za Mkoa wa Dodoma, Viongozi wa CCM na Waandishi wa Habari.

Akitoa salamu zake wakati wa kukabidhi ofisi, Ndg. Rugimbana amemshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa Imani kubwa aliyokuwa nayo kwake tangu alipomteuwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Dodoma hadi alipoamua kufanya mabadiliko kwenye safu ya Wakuu wa Mikoa Oktoba 26, 2017 na kuahidi kuwa akiwa uraiani ataendelea kulitumikia Taifa na kuiunga mkono Serikali, lengo likiwa kuhakikisha azma ya Serikali ya awamu ya tano inatimia.

“Pamoja na mabadiliko haya ya Uongozi, daima nitaendelea kukienzi na kukiishi kiapo cha uongozi nilichokula. Aidha, nitaendelea kulitumikia Taifa kwa nguvu zangu zote na kuiunga mkono Serikali ya Awamu ya Tano ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inayoongozwa na Rais Dkt. John Pombe Magufuli” alisisitiza Ndg. Rugimbana.

Pia alishukuru kwa ushirikiano alioupata kutoka kwa taasisi na wadau mbalimbali Mkoani Dodoma wakati wote wa uongozi wake na kuomba ushirikiano huohuo uendelezwe kwa Mkuu mpya wa Mkoa wa Dodoma Mheshimiwa Dkt. Mahenge. Pamoja na salamu hizo, Ndg. Rugimbana alimkabidhi Dkt. Mahenge taarifa rasmi ya Makabidhiano yenye Mikakati ya shughuli mbalimbali za maendeleo kwenye Mkoa iliyojumuishia masuala mbalimbali kama Ujio wa Serikali Mkoani Dodoma, Kilimo, Viwanda, Biashara, Uwekezaji na huduma za jamii.

Kwa upande wake Mkuu mpya wa Mkoa wa Dodoma Mheshimiwa Dkt. Bilinith Mahenge amesema akiwa Mkoani Dodoma atahakikisha azma ya Rais Magufuli ya Tanzania ya Viwanda inafanikiwa, vilevile atahakikisha anasimamia na kufuatilia shughuli zote za maendeleo kwenye Mkoa, ameomba ushirikiano mkubwa kutoka kwa viongozi mbalimbali Mkoani Dodoma, wadau na wananchi wote ili kuwa timu moja katika kujiletea maendeleo na ametaka kupitia ushirikiano huo kuhakikisha kero na changamoto za wananchi zinamalizwa.


Jeremiah Mwakyoama

Afisa Habari na Uhusiano
OFISI YA MKUU WA MKOA - DODOMA
Oktoba 30, 2017